**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA FEDHA**

# BODI YA WATAALAM WA UNUNUZI NA UGAVI

# TAARIFA KWA UMMA

## USAJILI WA MITIHANI YA 31 YA PSPTB (MID SESSION EXAMINATIONS)

**Dododa 03 Julai, 2025.**
Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB) inapenda kuwajulisha wadau wake kuwa, inatarajia kuendesha mitihani ya kitaaluma ya 31 ya PSPTB kuanzia tarehe 25/08/2025 hadi tarehe 29/08/2025. Waombaji wenye sifa na nia ya kuomba kufanya mitihani hii wanaelekezwa kufanya usajili wa mitihani hii kupitia **https://registration.psptb.go.tz** na pia kuhudhuria madarasa ya mafunzo kama sehemu ya maandalizi ya mitihani hiyo. Mitihani hii itafanyikia katika kituo kimoja kilichoko Dodoma kama inavyooneshwa katika dirisha la usajili na mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 15/08/2025.

**Waombaji wenye sifa ya kufanya mitihani ya kitaaluma ya agosti, 2025**

(a) Wahitimu wote waliomaliza Vyuo vya Elimu ya Juu na Kati kwa ngazi za Shahada, Stashahada na Astashahada ya Ununuzi na Ugavi kwa kipindi cha kuanzia 2024 kurudi nyuma ambao hawakuwahi kufanya mitihani ya kitaaluma ya Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi.

(b) Wafanyakazi wote wanaofanya kazi za Ununuzi na Ugavi katika sekta binafsi na umma pasipokuwa na cheti cha CPSP.

(c) Wahitimu wenye taaluma nyingine nje ya ununuzi na ugavi kwa ngazi za stashahada shahada na Astashahada au wenye sifa za kitaaluma kutoka Bodi/Mabaraza ya taaluma husika na yanayotambulika na PSPTB.

(d) Watahiniwa wa PSPTB waliomaliza mitihani ya kitaaluma ya Awali ngazi ya pili (Basic Stage II), mitihani ya kitaaluma ngazi ya Msingi (Foundation Stage I and II), Mitihani ya Kitaaluma ngazi ya kwanza, pili, tatu na nne (Professional Stages I, II, III and PIV) ndani ya miaka mitano kwa mujibu wa matakwa ya Mtaala wa Kitaaluma.

(e) Watahiniwa wote wanaorudia baadhi ya masomo katika ngazi mbali mbali ndani ya miaka mitatu kwa mujibu wa matakwa ya Mtaala mpya.

*Mkandarasi Place, Ghorofa ya 7, S.L.P. 2663, Dodoma. Simu: +255 22 2865860 Nukushi: +255 22 2862138. Tovuti: http://www.psptb.go.tz.*
*Barua pepe: barua@psptb.go.tz*

**NB.**

(i) Watahiniwa wanaorudia mitihani zaidi ya ngazi moja wanaruhusiwa kuunganisha ngazi mbili zinazofuatana (Two Consecutive Blocs) kwa masomo kuanzia mawili hadi sita tu, na kwa kuzingatia ratiba ya mitihani ya 31 ya PSPTB. Hivyo, wanaombaji wote wanashauriwa kuangalia ratiba ya mitihani kabla ya kuomba kufanya mitihani hiyo.

(ii) Ada za mitihani tajwa zimewekwa kwenye tovuti ya PSPTB.

(iii) Uendeshaji wa mitihani mingine inayofanyika Novemba na Mei itaendelea kama kawaida.

Kwa maelekezo au ufafanuzi zaidi tafadhali piga simu namba **0738441972** au tuma barua pepe kupitia **examinations@psptb.go.tz**

**Imetolewa na :**

Digitally Signed By Godfred B. Mbanyi
Thu Jul 03 11:25:30 EAT 2025

Godfred B. Mbanyi

**MKURUGENZI MTENDAJI**